Mkwawa Journal of Education and Development, Vol. 4 (1): 101-117

Matumizi ya mbinu za kisanaa katika kutafsiri lugha ya ishara: Mifano kutoka riwaya ya *Shetani Msalabani*

Birigitha Ngwano John

Jinsi ya kurejelea makala hii: John, B.N. (2020). Matumizi ya mbinu za kisanaa katika kutafsiri lugha ya ishara: Mifano kutoka riwaya ya Shetani Msalabani. Mkwawa Journal of Education and Development, 4(1): 101-117. DOI: https://doi.org/10.37759/mjed.2020.4.1.5

Link to this article: https://doi.org/10.37759/mjed.2020.4.1.5

Mkwawa Journal of Education and Development, Vol. 4 (1)
ISSN: 2453-6040 (Print)
eISSN:2453-6059 (Online)
https://doi.org/10.37759/mjed.2020.4.1.5

Matumizi ya mbinu za kisanaa katika kutafsiri lugha ya ishara: Mifano kutoka riwaya ya *Shetani Msalabani*

Birigitha Ngwano John
Chuo Kikuu cha Dodoma
birigithangwano@gmail.com

Ikisiri

Kazi mbalimbali za kisanaa ikiwamo fasihi, husukwa kwa kutumia lugha ya ishara ambayo huibua maana mbalimbali kwa wasomaji. Makala hii inamulika mbinu za kisanaa zilizotumika kutafsiri lugha ya kiishara katika riwaya ya Shetani Msalabani iliyotafsiriwa kutoka katika lugha ya Kiingereza na Ngugi wa Thiong'o. Pamoja na wataalamu mbalimbali kutafiti kuhusu matatizo ya tafsiri, bado tafsiri ya kifasihi haijafanyiwa tafiti za kutosha hususan katika lugha ya Kiswahili. Tafiti nyingi zimekitwa katika matatizo ya tafsiri kwa ujumla. Wataalamu mbalimbali wa tafsiri, hususan za kifasihi wametafiti kuhusu mbinu, nadharia na matatizo ya kutafsiri matini za kifasihi. Aidha, suala la mbinu za kisanaa zinazotumika kutafsiri lugha ya ishara katika kazi za kifasihi halijashughulikiwa vilivyo. Lengo la makala hii ni kuchambua mbinu za kisanaa ambazo hutumiwa na mfasiri katika kujenga lugha ya ishara katika kazi ya fasihi. Data za makala hii zilitokana na mbinu ya usomaji matini iliyohusisha matini chanzi, matini lengwa na vyanzo vingine vya taarifa kama vitabu, tasinifu, majarida, makala na vyanzo vya mtandao vimesomwa. Mjadala wa data uliongozwa na Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano. Makala hii imebaini kuwa, mfasiri hutumia mbinu mbalimbali za kisanaa katika kutafsiri lugha ya ishara katika kazi za kifasihi. Mbinu hizo ni kama vile utomeleaji, motifu ya safari na tamathali za semi.

Historia ya Makala:

Kupokelewa: 05 Januari 2020

Kukubaliwa: 25 Julai 2020

Maneno muhimu:

Lugha ya ishara

Mbinu za kisanaa

Tafsiri

Shetani Msalabani

Utangulizi

Tafsiri ni uhawilishaji wa mawazo, taarifa na ujumbe wa maandishi kutoka lugha chanzi (LC) kwenda lugha lengwa (LL) (Mwansoko, Mekacha, Masoko & Mtesigwa, 2006). Kutokana na fasili hiyo, katika makala hii, tafsiri inatazamwa kama mchakato wa kuhawilisha mawazo yenye wasifu wa kifasihi kutoka LC kwenda LL. Tafsiri ya kifasihi hufanywa katika tanzu mbalimbali za fasihi andishi kama vile riwaya, tamthiliya na ushairi. Katika fasihi andishi, tanzu za riwaya na tamthiliya kwa idadi kubwa zimefanyiwa tafsiri kuliko utanzu wa ushairi (Mekacha, 2013). Riwaya mbalimbali zihusuzo fasihi zilizotafsiriwa kwa Kiswahili ni pamoja na riwaya ya *Shetani Msalabani* na *Barua Ndefu kama Hii*. Sababu za kutafsiri kazi za kifasihi ni pamoja na kueneza fasihi ya lugha fulani na utamaduni wake (Yegon, 2016).

Zoezi la kutafsiri matini za kifasihi si kazi rahisi kwa sababu linakumbana na changamoto mbalimbali kama vile tofauti za kitamaduni baina ya lugha mbalimbali (Malangwa, 2010). Pia, mbali na changamoto za kiutamaduni, zoezi la kutafsiri matini za kifasihi hukumbana na changamoto, hasa katika uzingativu wa usanaa uliopo katika matini chanzi (MC). Matumizi ya ishara ni kipengele kimojawapo katika uhakiki wa matumizi ya lugha katika fani ya fasihi. Kipengele hiki cha fani hufanya kazi mbalimbali katika kukuza na kujenga maudhui ya kazi husika. Matumizi ya ishara hujengwa kitamathali, hususani kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa kama vile sitiari na tashibiha. Ujenzi huu hufanyika kwa lengo la kuifanya kazi ivutie katika kusoma, kufikisha ujumbe na kuonesha weledi wa mwandishi katika usanaji wa kazi (Mosha, 2017). Utumizi ya lugha ya ishara katika tafsiri ya kifasihi usipozingatiwa ipasavyo, unaweza kusababisha ukiushi wa ujumbe uliosukwa kisanaa kushindwa kuwafikia wasomaji na hivyo kazi husika kupoteza ladha ya kifasihi. Hivyo, makala hii imelenga kumakinikia kipengele hicho cha uhawilishaji wa matumizi ya lugha ya ishara katika kazi za fasihi.

Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano

Mjadala katika makala hii unaongozwa na Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano. Nadharia hii imeasisiwa na Nida (1964) na baadaye kuendelezwa na wataalamu wengine ambao ni Catford (1965), Nida na Taber (1969) na Reiss (1971/ 2000). Jilala (2016) anasema kuwa Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano ni mkabala unaosisitiza ulinganifu katika ujumbe na mtindo baina ya LC na LL. Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano ni nadharia ya kwanza ya tafsiri ya kimawasiliano ambayo inalenga kuondoa tofauti zilizokuwepo baina ya utamaduni na isimu katika tafsiri. Nadharia hii imeleta mapinduzi katika tafsiri na hivyo kuifanya tafsiri

kuwa zoezi la kisayansi. Jambo muhimu linalosisitizwa na nadharia hii ni kuleta athari sawa kwa hadhira ya ML kama ilivyo kwa hadhira ya MC.

Nadharia hii ina mihimili mikuu mitatu ambayo ni; mosi, usomaji na uelewekaji. Mhimili huu unasisitiza kuwa MC lazima izingatie usomekaji kwa maana ya kusikika vema kwa wasomaji na kuwasilisha taarifa au maudhui pamoja na mtindo. Pili, uasilia na ufafanuzi ambayo ina maana kuwa matini iliyotafsiriwa inatakiwa isomeke kana kwamba, imeandikwa katika LL hiyo. Tatu, uzingativu wa athari sawa ambao unahusisha wasomaji wa ML kupata athari sawa kama ilivyo kwa wasomaji wa MC. Hivyo, katika makala hii, imetumika Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano katika kubainisha mbinu za kisanaa zilizotumika kutafsiri lugha ya ishara katika *Shetani Msalabani*. Makala hii imetumia nadharia hii kwa sababu inasisitiza mfasiri kuzingatia ulinganifu wa kimawasiliano katika tafsiri ya matini za kifasihi bila kupoteza vipengele mbalimbali vya kisanaa katika kazi husika. Hii ni kwa sababu matini za kifasihi hutumia lugha ya kisanaa hivyo mfasiri ana wajibu wa kumfanya msomaji wa MC apate ladha ya kifasihi katika kazi anayoisoma.

Muhtasari wa Riwaya ya *Shetani Msalabani*

Shetani Msalabani ni riwaya iliyotafsiriwa kwa Kiswahili kutoka riwaya ya *Devil on the Cross* na Ngugi wa Thion'go mwaka 1982. Awali, riwaya hii iliandikwa kwa lugha ya Gikuyu kama *Caitani Mutharaba-ni* na baadaye akaitafsiri kwa lugha ya Kiingereza kama *Devils on the Cross* (Thion'go, 2013). Tafsiri ya Kiswahili ilitoka katika matini ya lugha ya Kiingereza na tafsiri hii ilifanywa pia na Ngugi wa Thion'go ambaye pia ndiye mwandishi. Riwaya hii ni hadithi ya wazalendo wanne ambao ni wa wakike wawili, Wariinga na Wangari, na wa kiume ni Muturi na Gatuiria. Wote wanasafiri katika matatu ya Mwaura wakielekea Ilmorog kujionea mashindano ya wizi na unyang'anyi wa kisasa. Wakati wakiwa safarini walijadili matatizo mbalimbali ambayo huonesha udhalimu, unyanyasaji na matabaka yaliyopo nchini Kenya. Safari yao imebeba pande mbili zinazovutana. Upande unaotetea tabaka tawaliwa ukiongozwa na Wariinga pamoja na Wangari na upande unaotetea tabaka tawala unaoongozwa na dereva Mwaura. Safari yao inaakisi mapito ya kihistoria nchini Kenya baada ya uhuru kwa kuangazia ukoloni mamboleo. Kupitia safari hiyo, tunaona namna viongozi wa nchi zinazoendelea wanavyoshirikiana na mabeberu kuwanyonya wafanyakazi na wakulima. Lengo la muhtasari huu wa riwaya ya *Shetani Msalabani* ni kumsaidia msomaji wa makala hii kufahamu kwa ufupi kuhusu riwaya teule.

Mbinu za Kisanaa Zilizotumika Kutafsiri Lugha ya Ishara katika *Shetani Msalabani*

Sehemu hii imejikita katika kuibua na kujadili mbinu za kisanaa zilizotumika kutafsiri lugha ya Ishara katika *Shetani Msalabani*. Mjadala huu umeongozwa na Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano inayotumika kuhakiki kazi za tafsiri**.** Mbinu muhimu zinazojadiliwa ni utomeleaji, motifu ya safari na tamathali za semi kama ifuatavyo:

Utomeleaji

Hii ni mbinu ya kisanaa ambayo huhusisha uchopekaji wa vipande vya utanzu mwingine ambao ni tofauti na utanzu unaoshughulikiwa (Ponera, 2014). Mbinu hii hujulikana pia kama mwingiliano tanzu. Utafiti umebaini kuwa, mfasiri wa riwaya teule ametumia mbinu hii ya kisanaa katika kutafsiri lugha ya ishara kwa kutumia mbinu nyingine ndogo ndogo ambazo ni:

Matumizi ya Methali

Methali ni semi fupi zilizosheheni fumbo juu ya ukweli wa maisha ya binadamu na huwa na umbo maalumu (Simiyu, 2013). Hizi ni semi za kimapokeo ambazo hutumia maneno ya kawaida kabisa kwa namna ya kufumba jambo linalohusu ukweli fulani wa maisha ya kila siku. Utafiti umebaini kuwa, mfasiri ametumia baadhi ya methali katika tafsiri kwa namna ya kuwakilisha lugha ya ishara. Kwa mfano katika methali ifuatayo:

1. **LC:** And Kareendi now knows only too well that no one repents on account of other sins. There is no one who regrets the going as much as the returning. To be smiled at is not to be loved (uk. 18).

   LL: "Tuseme huyu Kaledi amejifunza kuwa **mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe**. Baada ya kishindo kilio! Amejua ya kuwa na anayekuchekesha siye rafiki" (uk. 16).

Katika mfano namba 1, mfasiri ametumia methali ya "mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe" ambayo haikutajwa kwa namna ya moja kwa moja katika LC. Tafsiri hii imefanyika kwa kuzingatia msingi wa Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano unaohusisha uasilia na ufafanuzi. Fasihi iliyotafsiriwa inatakiwa isomeke kana kwamba imeandikwa katika LL hiyo. Methali ya "mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe" ina maana kuwa rafiki wanaokupenda wakati wa raha wanaweza wasishiriki nawe katika shida zako. Methali hii imewakilisha lugha ya ishara ambayo imekitwa kwa Jacinta Wariinga kama mhusika mkuu katika riwaya hii. Wariinga

alikumbana na magumu mno ya kimaisha hususani pale ambapo alipewa ujauzito akiwa kidato cha pili, kisha kukataliwa na mwanaume huyo. Hata hivyo, Wariinga hakupata msaada wa karibu kutoka kwa marafiki zake aliokuwa anafurahi nao wakati wote.

Aidha, kuna methali nyingine iliyotumika kutafsiri lugha ya ishara katika riwaya teule. Hii imejitokeza pale Wariinga anapotaka kurubuniwa na rafiki zake ili aachane na mchumba wake kijana. Rafiki hao wanataka Wariinga ajihusishe na mahusiano na wanaume wengine. Wariinga ni mweledi wa kubaini athari zijitokezavyo katika suala la mwanamke kuhusiana na wanaume wengi ndiyo maana akawajibu kwa kutumia methali hii, anasema:

> **2.** **LC**: They taunt her: "A restricted diet is monotonous." Kareendi rejects this and tells them: "**A borrowed necklace may lead to the loss of one's own**" (uk. 20).
>
> **LL**: Wakamjibu hivi na vile, 'Chakula cha aina moja miaka nenda miaka rudi hakifai.' Kaledi akawajibu, '**Usiache mbachao kwa msaala upitao**' (uk. 19).

Katika mfano namba 2, *A borrowed necklace may lead to the loss of one's own* imetafsiriwa kuwa "usiache mbachao kwa msaala upitao". Mfasiri ametumia methali hiyo tofauti na namna ilivyo katika LC kutokana na ukweli kuwa methali hutofautiana baina ya lugha mbalimbali. Hivyo, mfasiri kulingana na Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano hutafuta methali ya lugha ya Kiswahili ambayo inakaribiana kimaana na ile iliyotumika katika LC ili kupata athari sawa kwa wasomaji. Methali ya "usiache mbachao kwa msaala upitao" imetumika kama mbinu ya kisanaa ya kutafsiri lugha ya ishara katika riwaya teule. Kwa kawaida, neno mbachao ni kifaa kikuukuu kinachotumika kufanyia ibada mathalani mkeka au jamvi. Pia, neno msala hutumika kuwakilisha kifaa kizuri cha kufanyia ibada ambacho huwa bora kikilinganishwa na mbachao. Methali hii ina maana kuwa usije kuacha vitu au watu wako wa kudumu kwa kurubunika kwa mambo yanayopita ama starehe za muda mfupi.

Aidha, methali hii "usiache mbachao kwa msaala upitao" inaashiria uaminifu wa Kalendi kwa mchumba wake kijana John Kimwana na hataki kurubuniwa kwa namna yoyote kwa kuwa yeye ameridhika na maisha yake. Kalendi alishapata funzo kwa mara ya kwanza pale alipotiwa mimba akiwa katika kidato cha pili tu. Hivyo, hii kwake ni fundisho tosha.

Matumizi ya Hadithi

Hadithi ni utanzu wa fasihi simulizi ambao unahusisha masimulizi au tungo ndefu za kubuni au za kweli zinazotongolewa kwa lugha ya nathari au ya moja kwa moja (Simiyu, 2013). Matumizi ya hadithi mbalimbali katika riwaya teule yametumika kama mbinu ya kisanaa ya utomeleaji iliyotumika kutafsiri lugha ya ishara. Mbinu hii ya masimulizi imedhihirika kupitia namna zifuatazo:

Matumizi ya Mbazi

Mbazi ni hadithi fupi fupi zenye mafunzo maalum katika jamii ambazo hutolewa kama kielelezo wakati wa maongezi au wa kumkanya mtu (Mulokozi, 2017). Aghalabu, mbazi ni hadithi zenye kutumia lugha ya ishara ambayo huhitaji tafakuri ili kubaini maana iliyokusudiwa. Mifano ya mbazi ni zile zilizotolewa na Yesu Kristo katika Biblia kama mbazi ya msamaria mwema, mwana mpotevu na bwana harusi. Mbinu hii imetumika katika tafsiri ya *Shetani Msalabani* kupitia hadithi ya Mwireri wa Mukiraai ambaye anasema:

1. **LC:** '…For the kingdom of Heaven is as a man travelling into a far country, who called his own servants, and delivered unto them his goods. And unto one he gave five talents, to another two, and to another one...' (uk. 81).

   LL: Tazama, ufalme wa mbinguni unaweza kufananishwa na mtu aliyetaka kusafiri akawaita watumwa wake akawakabidhi mali yake. Akampa mmoja talanta tano, na mmoja talanta mbili, na mmoja talanta moja… (uk. 104).

Mfano huo namba 1 unadhihirisha mbazi ya mtawala aliyewapa watumwa wake mali yake wamlindie na kuendelea kumvunia. Akampa mtumwa mmoja shilingi laki tano, mwingine laki mbili na mwingine laki moja. Mtumwa wa kwanza aliyepewa shilingi laki tano alienda kununua vyakula kwa bei nafuu kwa wakulima wadogowadogo na kuuza mjini kwa bei kubwa na kisha kupata faida ya shilingi laki tano. Mtumwa wa pili aliyepewa shilingi laki mbili akafanya hivyo hivyo na akajipatia faida ya shilingi laki mbili. Lakini yule mtumwa aliyepewa shilingi laki moja akajifikiria sana na kuzifukia fedha alizopewa bila ya kupata faida yoyote. Basi ikafika siku ambayo mtawala akarudi kuona kitu kilichofanyika kwa watumwa wake. Akawapongeza wale watumwa wawili waliopata faida na kumwita mtumwa wa tatu kuwa ni mtumwa mbaya kwa kuwa hajazalisha kitu chochote.

Pia, katika Biblia kuna mifano mengine ya mbazi kama vile mbazi kutoka Luka 8: 4-15 inayosema "Ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi..." Katika hadithi ya Mwireri wa Mukiraai anaendelea kusema:

2. **LC**: …For the Kingdom of Earthly Wiles can be likened unto a ruler who foresaw that the day would come when he would be thrown out of a certain country by the masses and their guerrilla freedom fighters... (uk. 82).

LL: Tazama, ufalme wa hila humu duniani unaweza kufananishwa na mtawala mmoja aliyefahamu mapema kwamba siku moja atafukuzwa na wazalendo mashujaa wa vita vya uhuru atolewe katika nchi hiyo… (uk. 105).

Data hiyo namba 2 inatumika kuonesha mbazi inayoonesha lugha ya ishara kwa kutumia mfano wa ufalme wa hila duniani na mtawala mmoja. Kupitia mbazi hii tunapata maana mbalimbali kutokana na ishara zilizotumika. Mtawala anawakilisha wakoloni ama mabeberu ambao kwao walitaka faida kutoka katika nchi walizozitawala na hivyo kupandikiza mizizi ya ukoloni mamboleo. Watumwa wawili waliozalisha faida ni viongozi ambao wanashirikiana na wakoloni katika kuwagandamiza watu wanaowaongoza. Na hivyo wanapendwa na wakoloni hao. Mfano pale mtawala anaposema:

3. **LC:** 'As for you, from now on I shall no longer call you slaves or servant in public. Now you are truly my friends. Why? Because even after I had given you back the keys to your country, you continued to fulfil my commandments and to ptotect my property, making my capital yield a higher rate of profit than was the case when I myself used to carry the keys (uk. 86).

LL: Nanyi kutoka leo sitawaita watumwa wangu hadharani" Kutoka leo ninyi ni marafiki zangu; mmeendelea kutii amri zangu za kuulinda na kuukuza utajiri wangu hata kuliko vile nilivyoweza kufanya mwenyewe nilipokuwa na ufunguo wa hii nchi yenu (uk. 111).

Mfano namba 3 unaonesha kuwa viongozi hao wasaliti bado wanaendelea kutii na kuzilinda mali zilizopo nchini kwao kwa manufaa ya wakoloni/ mabeberu kutoka mataifa yaliyoendelea na hii ndiyo dhana halisi ya ukoloni mamboleo. Aidha, mtumwa wa tatu anawakilisha baadhi ya Waafrika ambao wameshagundua njama za wakoloni na hawataki kushirikiana nao na hivyo

hawapendwi na wakoloni hao kwa kuwa tu hawawazalishii faida. Mfano huu wa mbazi unalandana na ule unaopatikana katika biblia kwenye kitabu cha Mathayo 25:14-30 kuhusu talanta.

Hapa tunaona kuwa mbazi hii inawakilisha nchi zilizotawaliwa ikiwemo Kenya ambayo ndiyo inazungumzwa kwenye hii riwaya. Ukoloni umeoneshwa kwa kutumia ufalme wa hila humu duniani na namna wakoloni walivyojua kuwa ipo siku wataondolewa katika nchi hizo. Hali hii inathibitika kupitia harakati za kupigania uhuru zilizofanyika ili kuwafukuza wakoloni hao. Jambo hilo liliwakasirisha wakoloni hao na ndipo walipoamua kuanza kutafuta njia za kuwafanya waendelee kuwatawala Waafrika.

Hadithi ndani ya Hadithi

Katika tafsiri ya *Shetani Msalabani*, imebainika kuwa kuna utumiziwa mbinu ya kisanaa ya hadithi ndani ya hadithi ambao umetumika katika namna zifuatazo. Mosi, kuna hadithi ambayo mama Wariinga anamwambia mcheza ngoma ya Gicaandi aisimulie kwa watu ili waijue na wajifunze, anasema:

4. **LC:** And then Wariinga's mother came to me when dawn was breaking, and in tears she beseeched me: Gicaandi player, **tell the story of the child I loved so dearly** (uk. 7).

   LL: Siku moja wakati wa mapambazuko mamake Wariinga alikuja kwangu akanishawishi sana, huku machozi yanamlengalenga: Ewe mcheza ngoma ya Gicaandi, **itoe hadithi ya huyo mwanangu niliyempenda sana** (uk. 2).

Kifungu cha maneno *tell the story of the child I loved so dearly* kimetafsiriwa kuwa "itoe hadithi ya huyo mwanangu niliyempenda sana". Tafsiri hii inadokeza namna mama Wariinga alivyokuwa na huzuni ndiyo maana machozi yanamlengamlenga pia anasisitiza kuwa hadithi ya mwanawe anayempenda iweze kusimuliwa. Utafiti umebaini kuwa, maneno "hadithi ya mwanangu niliyempenda sana" yametumia lugha ya ishara inayowakilisha historia ya Kenya baada ya uhuru iweze kusimuliwa bila woga ili watu waifahamu. Watu wajue kuwa ukoloni haukuondoka bali umekuja kwa namna nyingine.

Pili, hadithi ndani ya hadithi imetokea pale Jacinta Wariinga anaposimulia hadithi ya Maua Kaledi. Anasema:

5. **LC:** Take a girl like me, 'Wariinga said gazing down at one spot as if she were talking to herself. 'Or take any other girl in Nairobi. Let's call her Mahua Kareendi (uk. 17).

> **LL**: "Chukua mfano wa msichana kama mimi" Wariinga akasema huku anatazama chini kama kwamba anasema peke yake' "Au chukua mfano wa msichana mwingine wa hapa Nairobi. Hebu tumwite Maua Kaledi (uk. 14)

Data namba 5 inaonesha jinsi Jacinta Wariinga anavyoanza kusimulia hadithi kwa kumtumia mhusika mwingine wa kubuni anayeitwa Maua Kaledi. Hadithi hii imetumia lugha ya ishara ambapo Maua Kaledi ametumika kumwakilisha Wariinga mwenyewe. Kwa maneno mengine, tunaweza kusema Wariinga anasimulia hadithi ya historia yake inayowakilishwa na mhusika Maua Kaledi. Katika hadithi tunaona suala kubwa linalojitokeza ni mambo mbalimbali ambayo aliyapitia kama vile kupata ujauzito katika umri mdogo na kupata madhila ya rushwa ya ngono. Katika hadithi tunamuona Kaledi anayemwakilisha Wariinga akipata ujauzito akiwa kidato cha pili na baada ya hapo wazazi wake wanaamua kumsaidia kumlelea mtoto na yeye anaamua kwenda kujiendeleza kielimu hadi kufika katika ngazi ya cheti katika chuo cha uhazili.

Matumizi ya Misemo

Miongoni mwa mbinu za kisanaa zilizotumika kutafsiri lugha ya ishara katika riwaya teule ni misemo ambacho ni kipera cha semi. Kipera hiki kinaendeleza hoja ya utomeleaji kwa sababu kimetumika katika riwaya ambayo ni tanzu ya fasihi andishi. Ponera na Kikula (2017) wanaeleza kuwa misemo ni vifungu vya maneno ambavyo hutumia lugha ya uficho kwa ajili ya kufikisha ujumbe fulani. Katika riwaya ya *Shetani Msalabani* kuna misemo mbalimbali ambayo mfasiri ameitumia kutafsiri lugha ya ishara kama ifuatavyo:

Mosi, kuna msemo uliotumika kueleza dhana ya rushwa ya ngono ambayo inaonekana pale Jacinta Wariinga anapokumbana na changamoto ya kupata kazi jijini Nairobi. Siku moja Wariinga anakutana na mkurugenzi mmoja wa kampuni, msimulizi anasema:

1. **LC:** Sister Kareendi, the case of a fool takes a long time to settle. Sister Kareendi, every court session opens with feasting. Sister Kareendi, no man licks an empty hand. **Take care of me, and I will take care of you**. (uk.19).

> **LL**: Dada Kaledi, **nipe nikupe**. Dada Kaledi, tumbo kwanza. Dada Kaledi mkono mtupu haurambwi.Nifae nami nikufae (uk.18).

"Nipe nikupe"ni msemo ambao umetumiwa na mfasiri kwa namna ya kutafsiri kifungu cha maneno *take care of me, and I will take care of you*. Msemo huu umetumika kuashiria mazingira ya rushwa ya ngono ambayo wanawake wengi kama Wariinga wanakutana nayo wakati wakiomba kazi.

Pili, msemo mwingine ulitumika pale rafiki wa Kaledi walipomuonea wivu kwa kuwa alipata mchumba wanayependana kwa dhati. Wanamwambia:

2. **LC:** Kareendi, you'd better change your ways: **the seeds in the gourd are not all of the same type**. (uk. 20)

   LL: Kaledi, **pombe si ya kitoma kimoja, badilisha** (uk. 19).

Msemo "pombe si ya kitoma kimoja, badilisha" umetumika katika kutafsiri lugha ya ishara. Ishara inayojitokeza hapa ni neno pombe ambalo limesimama badala ya mwanaume. Ikiwa na maana kuwa wanaume wanafaa kubadilishwa yaani mtu awe na mahusiano ya kimapenzi na wanaume wengi. Wariinga hakuwasikiliza rafiki zake kwa kuwa wanaonesha nia mbaya na wivu kwake.

Matumizi ya Nyimbo

Simiyu (2013) anaeleza kuwa nyimbo ni kipera cha fasihi simulizi kinachohusisha tungo zenye mapigo au mawimbi na huweza kuimbika. Nyimbo zina dhima mbalimbali kama vile kuelimisha, kuburudisha na kutunza amali za jamii. Wamitila (2003) anadokeza kuwa katika jamii za Kiafrika, nyimbo ni kipera kikongwe cha fasihi simulizi. Mfasiri ametumia nyimbo katika tafsiri kuwakilisha ishara mbalimbali. Kwa mfano, wakiwa kwenye matatu, Muturi na Wangari waliimba wimbo ufuatao:

1. **LC:** Kenya does not belong to you, imperialist!
   Kenya does not belong to you, imperialist!
   Pick up your bags and go!
   The owner of homestead is in his way! (uk. 47).

   LL: Beberu Kenya si kwenu!
   Beberu Kenya si kwenu!
   Funga virago
   Mwenye nyumba ashafika (uk. 57).

Wimbo huo umetumia lugha ya ishara inayosisitiza uhuru wa Kenya. Kifungu cha maneno *pick up your bags and go* kimetafsiriwa kuwa "funga virago mwenye nyumba amefika". Neno *bags* lingeweza kutafsiriwa kuwa mabegi lakini mfasiri ametumia neno "virago" kwa namna ya kudunisha na

kufedhehesha. Hii inaonesha hisia tosha anayoipata msomaji anaposoma wimbo huu kuwa mabeberu hawaitajiki Kenya na wanatakiwa waondoke kwa namna yoyote ile.

Motifu za Safari

Mbinu nyingine ya kisanaa iliyotumika kutafsiri lugha ya ishara ni motifu za safari. Ponera (2014) anaeleza kuwa motifu ni mbinu ya kisanaa ambayo hutumiwa na watunzi wa kazi za kifasihi kama misukumo au miegamo ya kujengea miundo (fani) au maudhui ya kazi zao. Pia, Nyamsenda (2015) anadokeza kuwa motifu ya safari ni aina ya motifu ambayo watunzi huitumia katika kazi zao ili kutoa ujumbe fulani kwa kutumia dhana ya safari inayojirudia. Katika riwaya teule, motifu ya safari imetumika kama mbinu ya kiusimulizi kwa namna ya kutumia lugha ya ishara yenye kuleta maana mbalimbali. Kwa mfano, tunaona Wariinga akiianza safari kutoka Nairobi kwenda nyumbani kwao Ilmorog. Msimulizi anasema:

1. **LC**: When Wariinga saw that there no other vehicle bound for Ilmorog, she entered Mwaura's (uk. 33).

LL: Wariinga alipoona kuwa hapakuwa na gari jingine la Ilmorog isipokuwa la Mwaura, alikata shauri kulipanda (uk. 37).

Mfano namba 1 unaonesha namna safari ya Wariinga inavyoanza katika gari la Mwaura linaloitwa Matatu Matata Matamu. Baada ya Wariinga kuingia katika gari hilo tunaona namna Mwaura ambaye ndiye mmiliki wa gari hilo akilisifia sana kwamba ndilo gari zuri lakini kiuhalisi gari hilo linaonekana ni la zamani na limechakaa. Mwaura anasema:

2. **LC**: Just before she had finished reading all the ads, Wariinga saw the driver jump out and start praising his matatu, calling attention to it with words and songs that were intended to distract people's eyes from its decrepit condition. 'Get in, get into Matatu Matata Matamu Model T Ford and you'll find yourself in Limuru, Satellite, Naivasha,Ruuwa-ini, Ilmorog…(uk. 31)

LL: Mara akaanza kuisifu matatu yake kwa nyimbo ili awasahaulishe wasafiri uzee wa matatu hiyo. "Ingieni, ingieni ndani ya matatu matata matamu Ford T, kufumba na kufumbua mjione Limuru, Naivasha, Ruwaini, Ilmorog… (uk. 33).

Kwa kuzingatia Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano, mfasiri amefanikiwa kuzingatia msingi wa athari sawa katika tafsiri iliyotumia mbinu ya motifu ya safari kama katika LC. Mfano namba 2 unaonesha namna Mwaura anaisifia gari yake kwa kuwavuta abiria waweze kupanda ili wafike kwa haraka sehemu wanazoenda. Lakini kwa upande wa abiria, wengi wanaonekana kuilaumu gari hilo kuwa limechakaa. Hii tunaona pale msimulizi anaposema:

3. **LC**: But the matatu had a public relations officer in Mwaura. People would ask him: Mwaura, does this vehicle belong to the days of Noah? (uk. 32).

LL: Mwenyewe, Robin Mwaura, **aliitetea sana watu walipoilaumu hiyo matatu yake**. Walikuwa wakimwuliza: Hii matatu yako Mwaura iliungwa kati wa kizazi cha Nuhu? (uk. 35).

Tunaona kifungu cha maneno Mwaura akiitetea sana watu walipoilaumu hiyo matatu yake hakijatokea moja kwa moja katika LL. Mfasiri amefanya kukiongeza ili wasomaji wa ML waweze kuelewa hali halisi ya wasafiri wa matatu walivyochoshwa na usafiri huo licha ya Mwaura kuusifia. Tena tunaona baadhi ya wasafiri hao walimuuliza kwa namna ya kumdhihaki kuwa matatu hiyo ilitengenezwa wakati wa kizazi cha Nuhu kumaanisha siku nyingi.

Kutokana na mifano hapo juu, kupitia motifu ya safari tunapata lugha ya ishara ambayo ina maana mbalimbali. Utafiti umebaini kuwa, matatu matata matamu ni ishara yenye maana ya taifa la Kenya ambalo tangu uhuru halijaondokana na minyororo ya ukoloni mamboleo. Mwaura anawakilisha viongozi ambao kazi yao daima huwa ni kusifu taifa limepiga hatua kimaendeleo ama lipo huru lakini katika hali ya kawaida si hivyo. Wasafiri wa matatu hiyo wanawakilisha tabaka la wanyonge ambao daima wakiwa wananyanyasika kutokana na uongozi mbaya na kila mara wakijaribu kusema ukweli hakuna mtu anayeweza kuwasikiliza kilio chao.

Matumizi ya Tamathali za Semi

Katika kutafsiri, mfasiri amefanikiwa kutumia matumizi ya tamathali za semi kama mbinu ya kisanaa katika kueleza lugha ya ishara. Kwa mujibu wa Senkoro (1982) na Msokile (1992), tamathali za semi ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata sauti katika maandishi ama kusema. Katika riwaya teule, zifuatazo ni baadhi ya tamathali za semi zilizotumika:

Tashihisi

Tashihisi ni tamathali ya semi ambayo inavipa sifa ya uhai vitu visivyo na sifa ya uhai na uwezo wa kutenda au kuonekana kama kina uhai (BAKITA, 2015). Kwa mfano, mbinu hii imetumika pale Muturi anaposema:

1. **LC:** "**This country, our country, is pregnant**. What it will give birth to, God only knows…. Imagine! The children of us workers are fated to stay out in the sun, thirsty, naked (uk. 46).

   LL: "**Nchi yetu ina mimba**. Kitakachozaliwa hapana ajuaye isipokuwa Mungu…Ati kweli watoto wetu sisi wafanyakazi wawe wakiona kiu, njaanawawe wakivaa mavazi machache? (uk. 55).

Kifungu cha maneno "nchi yetu ina mimba"ni tashihisi kwa sababu nchi imepewa uwezo wa kupata mimba kama ilivyo kwa binadamu. Tunajua kuwa kwa binadamu ni mwanamke ndiye mwenye uwezo wa kupata mimba na kwa kawaida hudumu kwa muda wa miezi tisa ndipo aweze kuzaa ama kujifungua. Kitendo cha Muturi kusema kuwa nchi yao ina mimba kinaashiria kuwa nchi iko kwenye matatizo kama vile uongozi mbaya, usaliti, rushwa, unyanyasaji na matatizo mengine ambayo yanahitaji kusuluhishwa kwa haraka. Anaendelea kusema kuwa:

2. **LC:** What it lacks now is **midwife**. (uk. 46).

   LL: Mkunga ndiye ambaye hajapatikana (uk. 55).

Katika mfano namba 2, tunaona kuwa nchi ambayo ina mimba imekosa mkunga. Neno *midwife* limetafsiriwa kuwa ni "mkunga". Huyu ni mtu anayefanya kazi ya kuzalisha wanawake. Kitendo cha kukosekana kwa mkunga ni ishara kuwa hakuna mtu ama viongozi ambaye anaweza kuwaondolea matatizo nchini Kenya.

Sitiari

Mfasiri ametumia mbinu ya sitiari kutafsiri ishara mbalimbali hususani zile zenye mlengo wa mapenzi na ngono. Sitiari ni tamathali ya semi inayolinganisha vitu viwili bila ya kutumia viunganishi. Madumulla (2009) anashadidia kwa kusema kuwa vitu vinavyolinganishwa sharti viwe tofauti kitabia na kimaumbile. Kwa mfano, sitiari mbalimbali zimejitokeza pale Boss Kihara anapomshawishi Kaledi ili ahusiane naye kimapenzi. Anasema:

1. **LC:** "**Beautiful Kareendi, flower of my heart**. No one but you can type them" (uk. 21).

   LL: Kaledi mrembo, kifu la moyo wangu. Hapana mwingine anayeweza kuzipiga tapureta barua hizo isipokuwa wewe (uk. 20).

Kupitia dondoo namba 1, tunaona lugha ya ishara yenye maana ya kuonesha hisia za mapenzi alizonazo Boss Kihara kwa kaledi. Ndiyo maana anamfananisha na kifu la moyo wake yakiwa ni maneno ya huba. Hii inaonesha pia viongozi wengi hutumia maneno mazuri kuwalaghai wafanyakazi wao ili waingie kwenye mtego wa mapenzi kama anavyofanya Boss Kihara kwa Kaledi.

Pia, sitiari nyingine ambayo Boss Kihara aliitumia kwa Kaledi ni:

2. **LC: Please, Kareendi, little fruit of my heart**, listen to me carefully so that I may tell you beautiful things (uk. 22).

   LL: Kaledi, dawa ya moyo wangu.Tega sikio nikupashehabari nzuri (uk. 21).

Hapa tunaona kuwa kifungu cha maneno *Please, Kareendi, little fruit of my heart* kimetafsiriwa kuwa "Kaledi, dawa ya moyo wangu". Katika tafsiri Kaledi analinganishwa na dawa kitu ambacho hakijaonekana kwenye LL. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano, mfasiri anapaswa kuzingatia usomekaji wa ML kwa kuweza kubadili baadhi ya vipengele lakini kwa kuzingatia athari sawa kama ilivyo kwenye MC. Kaledi kuwa dawa ni sitiari inayomfananisha na kitu ambacho kinatibu maradhi au magonjwa mbalimbali. Boss Kihara amemwita Kaledi kuwa ni dawa ya moyo wake kwa maana ya kuonesha kuwa anampenda kwa dhati.

Dhihaka

Miongoni mwa tamathali za semi zilizotumika katika tafsiri ya lugha ya ishara katika riwaya teule ni dhihaka. Hii ni tamathali ya dharau na ina lengo la kumweka mtu katika hali duni kupita kiasi, lakini kwa mbinu ya kifumbo (Msokile, 1992).Tunaweza kusema kuwa dhihaka, aghalabu, hutumikakwa namna inayoleta ufedheheshwaji kwa mtu anayekusudiwa kwa namna ambayo si ya wazi wazi au bayana. Hali hii humfanya mlengwa kujisikia vibaya kwa namna ya kukerwa au kudharauliwa. Katika riwaya teule, kwa mfano, mbinu ya kinaya imetumika pale Mwaura anapomwambia Gaturia, anasema:

1. **LC:** I do not want any wrangling between us. **This vehicle does not run on urine** (uk.37).

   LL: "Sitaki kilele hapa mama. **Gari hili haliendeshwi kwa nguvu za mkojo!** (uk. 42).

Mwaura ambaye ndiye dereva na mmiliki wa matatu anakasirishwa na hali ya Gatuiria kutokuwa na nauli ya kulipa ndipo anapoamua kutumia dhihaka ya "gari hili haliendeshwi kwa nguvu za mkojo". Kama tunavyojua kuwa vyombo vya moto vya usafiri vikiwemo magari na pikipiki hutumia mafuta katika uendeshwaji wake kama mafuta ya petroli au dizeli ambayo hununuliwa kwa fedha. Mwaura anamdhihaki Gatuiria kwa kumwambia kuwa gari lake halitumii mkojo ambao kila mtu anaweza kuutoa bali hutumia mafuta yanayonunuliwa kwa fedha. Kauli hii inamdhalilisha Gatuiria kwa kumuonesha kuwa si mtu wa thamani na hapaswi kupanda gari ya Mwaura kitu ambacho kilisababisha akina Wangari, Waringa na abiria wengine wamchangie fedha ili Gatuiria asishushwe kwenye gari hilo. Kinaya hii imetumia lugha ya ishara yenye maana ya kuonesha namna viongozi wanavyowanyanyasa watu wa tabaka la chini kwa kuwaona kuwa si chochote na si lolote. Mwaura anawakilisha watu wa tabaka tawala yaani viongozi na Gatuiria anawakilisha watu wa tabaka la chini yaani watawaliwa.

Hitimisho

Kutafsiri kazi za kifasihi ni tofauti na kazi zisizo za kifasihi. Hii ni kutokana na ukweli kuwa kazi za kifasihi husanwa kwa kuzingatia sanaa na ubunifu wa hali ya juu. Ikiwa mfasiri si mweledi katika mbinu za kisanaa basi itakuwa ni vigumu kwake kuweza kutafsiri kwa namna inayofaa na kuleta tija kwa wasomaji wa LL. Makala hii imebaini kuwa mfasiri anayo nafasi yenye hadhi sawa na mwandishi katika utumizi wa lugha kisanaa. Kupitia *Shetani Msalabani*, tunaona utumizi wa lugha ya ishara umefanikishwa kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa ambazo zimeifanya ML ionekane katika umbo la kisanaa kama MC yake. Kupitia lugha iyo ya ishara, wasomaji wameweza kupata dhamira na ujumbe mbalimbali uliokusudiwa na mwandishi katika MC. Aidha, mfasiri amejitahidi kuzingatia misingi ya Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano ambayo hukitwa katika kuleta usomekaji, uelewekaji, uasilia na kuwepo kwa athari sawa.

Marejeleo

BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers.

Bible Society of Tanzania. (1997). *Biblia Takatifu*: Kitabu cha Mathayo 25: 14 -30. Dodoma: Bible Society of Tanzania.

Catford, J. (1965). *A Linguistic Theory of Translation*. London: Oxford University Press.

Jilala, H. (2016). "Uchambuzi wa Nadharia ya Ulinganifu katika Fasihi" katika Jilala, H. (Mh.). *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Limited.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers.

Malangwa, P. (2010). Handling Technical Translations: The Case of Translation of Computer Programs from English into Kiswahili." Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Isimu.Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (Haijachapishwa).

Mekacha, R. D. K. (2013). "Tafsiri ya Ushairi" katika Mwansoko, H. J. M na wenzake (2013). *Kitangulizi cha Tafsiri. Nadhania na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.

Mosha, D. (2017). "Lugha ya Ishara katika Dhifa za Jikoni (*Kitchen Party*) Nchini Tanzania" katika *Kioo cha Lugha* Juzuu 15 (1)uk. 145-157. Dar es Salaam: TUKI.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mulokozi, M. M. (2017).*Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU Ltd.

Mwansoko, H. J. M, Mekacha, R. D.K, Masoko, D. L. W & Mtesigwa, P. C. K. (2006). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadhania na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.

Nida, E. (1964). *Toward a Science of Translation*. Leiden: E. J. Brill.

Nida, E. & Taber, C. R. (1969). *The Theory and Practice of Translation*. Shanghai: Foreign Language Education Press.

Nyamsenda, J. C. (2015). Ushujaa wa Shujaa wa Motifu za Safari na Msako katika Ngano za Waikizu, Wabondei na Wazanzibari. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Kiswahili.Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa).

Ponera, A. (2014). *Utangulizi wa Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karl Jamer Publishers.

Ponera, A. S. & Kikula, I. S. (2017).*Misemo ya Vyombo vya Usafiri*. Dar es Salaam: Afroplus Industries Limited.

Reiss, K.(1971/2000). Moglichketeiten und Grenzen der Ubersetzungskrititik, Munich: M. Hubeber, imetafsiriwa na E. F. Rhodes (2000), kama *Translation Criticism: Potential and Limitations*. Manchester: St. Jerome and American Bible Society.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam Press and Publicity Centre.

Simiyu, W. F. (2013). *Kitovu cha Fasihi Simulizi*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Limited.

Wa Thiong'o, N. (2013).*Wasomi Lugha za Ulaya na Afrika:Kati ya Kujiweza na Kuwezwa*. Dar es Salaam: Mhadhara baada ya kutunukiwa Digrii ya Heshima ya Uzamivu (PhD) tarehe 23/11/2013.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Yegon, M.C. (2016). Uwasilishaji wa Ufeministi Kinzani katika Kiswahili Kupitia Tafsiri: Tathmini ya Riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*.Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu Cha Nairobi, (Haijachapishwa).